IB DIPLOMA PROGRAMME
PROGRAMME DU DIPLÔME DU BI
PROGRAMA DEL DIPLOMA DEL BI



**SWAHILI *AB INITIO* – STANDARD LEVEL – PAPER 1**
**SOUAHÉLI *AB INITIO* – NIVEAU MOYEN – ÉPREUVE 1**
**SUAHELI *AB INITIO* – NIVEL MEDIO – PRUEBA 1**

Thursday 8 May 2003 (afternoon)
Jeudi 8 mai 2003 (après-midi)
Jueves 8 de mayo de 2003 (tarde)

1 h 30 m

---

TEXT BOOKLET – INSTRUCTIONS TO CANDIDATES

- Do not open this booklet until instructed to do so.
- This booklet contains all of the texts required for Paper 1 (Text handling).
- Answer the questions in the Question and Answer Booklet provided.

LIVRET DE TEXTES – INSTRUCTIONS DESTINÉES AUX CANDIDATS


- Ne pas ouvrir ce livret avant d'y être autorisé.
- Ce livret contient tous les textes nécessaires à l'épreuve 1 (Lecture interactive).
- Répondre à toutes les questions dans le livret de questions et réponses.

CUADERNO DE TEXTOS – INSTRUCCIONES PARA LOS ALUMNOS

- No abra este cuaderno hasta que se lo autoricen.
- Este cuaderno contiene todos los textos requeridos para la Prueba 1 (Manejo y comprensión de textos).
- Conteste todas las preguntas en el cuaderno de preguntas y respuestas.

**KIFUNGU A**

# Mwisho wa Masomo




Wanafunzi watamaliza mitihani leo na jioni watakuwa na sherehe. Watakula, watakunywa, wataimba, watazungumza, na kucheza muziki pamoja na rafiki. Sherehe itaanza saa 12.30 jioni. Kwanza watakula chakula cha jioni. Pili watacheza michezo mbalimbali. Tatu, saa 2.00 usiku wataangalia na kucheza ngoma za utamaduni. Saa 4.00 usiku watacheza muziki wa disko. Saa 6.00 usiku watamaliza muziki na kwenda kulala.

**KIFUNGU B**

# Sherehe ya Kupata Shahada

*Baba yao Mwajuma na Ali anawaandikia barua rafiki zake kuhusu watoto wake hao ambao watakuwa na sherehe ya mahafali ya kumaliza digrii ya kwanza mwezi ujao.*



Makongo Juu,
S.L.P. 35091,
Dar es Salaam,
Tanzania.
Oktoba 30.


Wapendwa rafiki zangu wote,

Salamu nyingi kutoka hapa Makongo Juu. Ninatumaini kuwa wote hamjambo. Mimi na mke wangu na familia yangu yote hatujambo. Barua hii ni ya kuwakaribisha katika sherehe ya mahafali ya watoto wangu, Mwajuma na Ali, ambao watapata shahada yao ya kwanza ya B.A. mwezi ujao tarehe 26. Ningependa kuwaalikeni nyote katika sherehe hii ambayo itaanza saa tano asubuhi kule Chuo Kikuu cha Dar es Salaam katika Jumba la Mikutano la Nkrumah. Baada ya kutunukiwa shahada hiyo, wote tutakwenda nyumbani kwangu kwa sherehe. Hapa ninaambatisha ratiba ya sherehe pamoja na ramani ya jinsi ya kufika nyumbani kwangu Makongo Juu. Ninatumaini kuwa kila mmoja wenu ataweza kuja na kushiriki nasi katika kuwapongeza watoto wetu hawa kwa mafanikio yao ya kielimu.

Wasalaam,

*Shabani Rajabu*

**KIFUNGU C**




# KITABU CHA KUMBUKUMBU CHA JAMILA ALI

| Januari 2002 | | Shughuli |
|---|---|---|
| Jumanne | 1 | Sikukuu ya mwaka mpya -kuenda Arusha |
| Jumatano | 2 | Arusha – Mbuga za wanyama na rafiki zangu |
| Alhamisi | 3 | Arusha – Kupanda mlima Meru |
| Ijumaa | 4 | Arusha – Mlima Meru |
| Jumamosi | 5 | Arusha – Kupumzika hotelini – ***Hoteli ya Impala*** |
| Jumapili | 6 | Nairobi ***Hoteli ya Stanley*** |
| Jumatatu | 7 | Kupumzika na kumtembelea rafiki Alice Muthengi |
| Jumanne | 8 | Matembezi Nairobi: Bustani ya Nyoka |
| Jumatano | 9 | Kutembelea Kituo cha Utangazaji, KBC – Nairobi |
| Alhamisi | 10 | Mahojiano na Mkurugenzi wa KBC – Nairobi |
| Ijumaa | 11 | Kupumzika Nairobi na kuogelea hotelini. |
| Jumamosi | 12 | Safari ya Moshi, Tanzania |
| Jumapili | 13 | Kupumzika hotelini – Marangu Hotel |
| Jumatatu | 14 | Kupanda Mlima Kilimanjaro |
| Jumanne | 15 | Kupanda Mlima Kilimanjaro |
| Jumatano | 16 | Kupanda Mlima Kilimanjaro |
| Alhamisi | 17 | Kupanda Mlima Kilimanjaro |
| Ijumaa | 18 | Kupanda Mlima Kilimanjaro |
| Jumamosi | 19 | Kurudi hotelini na kupumzika – ***Marangu Hotel*** |
| Jumapili | 20 | Mapumziko na matembezi Moshi mjini |
| Jumatatu | 21 | Safari ya kurudi Dar es Salaam |
| Jumanne | 22 | Kupumzika nyumbani Mbezi Beach, Dar es Salaam |
| Jumatano | 23 | Kuwatembelea rafiki zangu Masaki na Oysterbay, Dar |
| Alhamisi | 24 | Madukani mjini Dar es Salaam asubuhi |
| Ijumaa | 25 | Nyumbani |
| Jumamosi | 26 | Disko |
| Jumapili | 27 | Kupumzika nyumbani: Sikukuu yangu ya kuzaliwa |
| Jumatatu | 28 | Kupumzika nyumbani |
| Jumanne | 29 | Nyumbani: Kujiandaa kwa safari |
| Jumatano | 30 | Nyumbani: kujiandaa kwa safari |
| Alhamisi | 31 | Safari ya Madison, Wisconsin, Marekani |

**KIFUNGU D**

# KUMKARIBISHA MGENI

*Mariamu na watoto wake wamepata barua kutoka kwa Moneera, rafiki wa kalamu. Moneera anasema atakuja kuwatembelea, lakini angependa kujua watavaa nini ili awatambue watakapowasili uwanja wa ndege. Zubeida amemwandikia Moneera barua-pepe kumweleza yeye na watoto wake watavaa nini.*

| | |
|---|---|
| ***kwa*** | moneera@yahoo.com |
| ***kutoka*** | zubeida_2@hotmail.com |
| ***tarehe*** | 12.08.02 |
| ***yahusu*** | Karibu Mombasa |
| ***n.k.*** | zuberi2002@ud.co.tz, samira_zx@aol.com |

Mpendwa Moneera,

Tunafurahi sana kusikia kwamba utakuja kututembelea hapa Mombasa.

Mimi na watoto wangu wawili, Zuberi na Samira tutakuja kukupokea uwanja wa ndege wa Mombasa hiyo siku utakapokuja. Kwa sababu hufahamu sura zetu, sasa ninataka kueleza tutavaa nini siku hiyo. Mimi nitavaa vazi la Kitanzania, yaani kitenge ambacho kina rangi nyekundu, njano na ya bluu kidogo. Pia kina maua mbalimbali. Hapa ninakutumia kiambatisho *(attachment)* cha picha yangu nikiwa nimevaa vazi hilo. Zuberi amesema kwamba yeye atavaa kanzu ya rangi nyeupe na kofia ambayo ni nyeupe vilevile. Bado sijajua Samira atavaa nini, lakini siku hizi anapenda sana kuvaa suruali nyeusi na blauzi ambazo ni ndogo na za rangi tofautitofauti. Nitaandika barua-pepe tena kueleza atavaa nini kwa sababu kwa sasa hayuko hapa nyumbani. Ninajua kuwa wewe, Samira na Zuberi mtafurahi kutoka kwenda kutembelea sehemu mbalimbali.

Salamu kwa baba na mama na wadogo zako. Je, utakuja mwenyewe?

Karibu sana Mombasa, Moneera.


Wako,

Mama Zuberi



**KIFUNGU E**

# SIKUKUU



**Sofia anamweleza rafiki yake kuhusu mipango yake ya Sikukuu.**

BAKARI: Habari gani Sofia?

SOFIA: Nzuri tu, na wewe je?

BAKARI: Nzuri sana. Sikukuu hii utafanya nini?

SOFIA: Sikukuu hii tutakuwa na shamrashamra nyingi sana nyumbani kwetu. Halafu pia ndugu zangu wanataka kunipongeza kwa kufaulu mitihani yangu.

BAKARI: Ehe, mtafanya nini?

SOFIA: Asubuhi na mapema nitakwenda sokoni kununua vitu mbalimbali.

BAKARI: Halafu?

SOFIA: Halafu nitarudi na wadogo zangu kupika. Tutapika vyakula vya aina mbalimbali.

BAKARI: Vyakula gani?

SOFIA: Tutapika pilau na wali mweupe kwa nyama na mbogamboga nyingi. Wadogo zangu wanapenda sana maandazi, kwa hiyo mama atakaanga maandazi na labda vitumbua na sambusa. Baba anapenda sana sambusa na bia. Na mama anapenda soda au mvinyo na pilau.

BAKARI: Baada ya chakula mtafanya nini?

SOFIA: Baada ya chakula cha jioni mimi na wadogo zangu tutaenda kutembea pwani hasa sehemu za Forodhani ambako kuna watu wengi. Lakini, kwa nini unauliza maswali mengi?

BAKARI: Nilitaka tutoke. Lakini hata hivyo, hongera sana kwa kufaulu mitihani yako, na sikukuu njema.

SOFIA: Asante sana. Na wewe sikukuu njema.

BAKARI: Asante sana sana.